Kwako Mbunge Mzalendo,

Kama unavyofahamu, kesho utashiriki kwenye mjadala muhimu kuhusu muswada wa mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa. Sisi marafiki zako kutoka asasi za kiraia tungependa kukufahamisha mambo machache ambayo pengine waandaji wa muswada hawajayaweka bayana. Mambo haya ni yale ambayo tunaamini yana madhara kwako na kwa chama chako katika shughuli zenu za kisiasa na maendeleo.

Awali ya yote, tungependa kubainisha malengo na maboresho muhimu ambayo yamependekezwa kwenye muswada huu ambayo nasi tunayaunga mkono bila shaka:

1. Vyama vya siasa vinaweza kuwajibika zaidi kwa wananchi kama baadhi ya vipengele vya muswada huu utatekelezwa kikamilifu.
2. Mabadiliko yaliyopendekezwa yanaweza kuchochea uzalendo na amani kwa Taifa kwa kuuwezesha umma kufahamu aina za mafunzo na misaada inayotolewa kwa vyama vya siasa.
3. Mabadiliko yaliyopendekezwa yanaweza kuongeza hali ya usalama kwa kila mtanzania na kurudisha jukumu la ulinzi kwa vyombo vya dola kama inavyopaswa kuwa.

Lakini, kama wahenga walivyonena, “penye urembo, pana urimbo”, tungependa kukufahamisha kuhusu mambo manne yaliyomo kwenye marekebisho ambayo ni hatari kwako, kwa chama chako na nchi yetu kwa ujumla.

1. Wanawake vijana na watu wenye ulemavu wamesahaulika kwenye marekebisho

Watu wenye ulemavu wametajwa mara moja tu kwenye marekebisho yote. Muswada huu hautoi malekezo kuhusu uwakilishi na ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika nafasi za uongozi za vyama vya siasa na katika kufanya maamuzi muhimu. Muswada huu ukipita, inaweza kupelekea wewe kama mgombea mtarajiwa kukosa fursa ya kuungwa mkono zaidi na kupata kura kutoka kwenye makundi haya na pia unakiuka tunu zetu za taifa ikiwemo kuvumiliana na ushirikishaji.

Tafsiri isiyo rasmi ya vipengele husika:
9(1) Chama hakitafuzu kupata usajili wa awali isipokuwa-
(c) – Uanachama wake ni wa hiari na uko wazi kwa wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano bila ubaguzi wa jinsia, ulemavu, imani ya dini, kabila, asili ya mtu, taaluma au kazi.

2. Hauruhusiwi kufanya kazi za kisiasa vyuoni, sehemu za ibada, na mahali pa kazi.

Licha ya kuzuiwa kufanya shughuli za kisiasa vyuoni, kanisani, msikitini na mahalipa kazi, ambayo itapelekea kukosa fursa za kujinadi na kupata kuungwa mkono, sheria hii haijaweka tafsiri ya nini maana ya “shughuli za kisiasa” na “mahali pa kazi”. Vile vile kukiuka vipengele hivi ni makosa yaliyowekewa adhabu kali. Hii inamaanisha wigo wako wa kufanya siasa kwa malengo yako binafsi na ya chama chako unakuwa umebanwa zaidi.

Tafsiri isiyo rasmi ya vipengele husika:
12 - (2) Kifungu kidogo cha (3) chama cha siasa au mtu yeyote haruhusiwi kufanya shughuli za kisiasa, kuunda, kuanzisha au kuruhusu uanzishaji au kuanzisha ofisi yoyote, tawi, umoja, shirika la vijana au wanawake au chombo kingine cha chama chochote cha siasa kwenye eneo la kazi, shule, sehemu nyingine za kutolea mafunzo, maeneo ya kuabudia, taasisi za serikali au umma.
12 - (6) Hairuhusiwi kutumia dini au mashirika ya kidini kuendeleza malengo ya chama cha siasa.

3. Vyama havitaruhusiwa kufanya kazi za ushawishi kwa serikali au umma kwa ujumla.

Mwanachama yeyote hataruhusiwa kwa mapendekezo haya kuishawishi serikali au kuhamasisha wananchi, kwa namna yoyote ile. Kwa mfano, mikutano ya hivi karibuni iliyofanyika Dodoma na Dar es

Salaam kujadili hali ya uchumi na siasa nchini, na karibu shughuli zote za hivi karibuni za katibu wa itikadi na uenezi wa chama tawala, zitakuwa kinyume cha sheria.

Tafsiri isiyo rasmi ya vipengele husika:
6A - (6): Chama cha siasa hakitafanya kazi kama kikundi cha uhamasishaji au cha kiharakati
(7) Kama kisemavyo kifungu kidogo cha (6), kikundi cha uhamasishaji au cha kiharakati kina maana ya kikundi cha watu ambao wanashawishi mitazamo ya umma na serikali ili ifanye jambo fulani kwa maslahi fulani.

4. Msajili ana mamlaka kuliko viongozi wa chama chako
Msajili anaweza kutengua au kusimamisha uanachama wa mwanachama yeyote bila kutoa sababu za msingi au ushahidi. Mwanachama anapokuwa amesimamishwa uanachama, hataruhusiwa hata kupiga kura kwenye uchaguzi wowote. Sheria hii inatoa mwanya kwa mtu yoyote kukufanyia fitna au hila ili kukuharibia kazi zako za kisiasa. Mbaya zaidi, muswada huu unampa kinga Msajili dhidi ya kupelekwa mahakamani kupinga maamuzi atakayoyachukua, kama vile kumsimamisha uanachama mwanachama yeyote.

Tafsiri isiyo rasmi ya vipengele husika:
21E - (1) Bila kuathiri mamlaka inayoelezwa kwenye Sheria hii, Msajili anaweza kumsimamisha mwanachama yeyote wa chama cha siasa ambaye amevunja kifungu chochote cha sheria hii kujihusisha na shughuli za kisiasa.
(2) Mwanachama yeyote ambaye atafanya shughuli za chama au za kisiasa au kushiriki kwenye uchaguzi wakati chama hicho kimesimamishwa, anatenda kosa.
6 – Hakuna mashtaka yatakayofunguliwa dhidi ya Msajili, Msajili Msaidizi, Mkurugenzi au maafisa wengine walioko chini ya Msajili kwa chochote kitakachofanywa au kutofanywa kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa jukumu lolote chini ya Sheria hii.

Japokuwa tuko pamoja katika kupongeza mabadiliko chanya yaliyomo kwenye marekebisho, tungependa uzingatie tuliyoyabainisha hapo juu pamoja na athari zake katika shughuli zako za kisiasa na maendeleo. Ni matumaini yetu kuwa tutazidi kushirikiana katika kujenga mfumo mzuri wa kisheria ambao utalinda usalama wa nchi na ustawi wa watanzania wote.

Kutoka

Centre for Strategic Litigation	Baraza la Habari	Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
Chama cha Wanasheria (TLS)	Twaweza	Waandishi wa Habari za Maendeleo